

## Maswali

1. Nani alikuwa mfalme wa milki kubwa ya Uajemi?
2. Mfalme Ahasuero alitaka malkia Vashti afanya nini?
3. Malkia Vashti alifanya nini?
4. Mfalme aliamua kufanya nini?
5. Mordekai alimlea nani?
6. Mbona Mordekai alipeleka Esta kwa jumba la mfalme?
7. Ahasuero alichagua nani kama malkia mpya?
8. Mordekai aliokoa uhai wa mfalme namna gani?
9. Jina la Mordekai liliandikwa wapi?
10. Mbona Mungu alikuwa akipanga haya yote?

## Majibu

1. Mfalme Ahasuero
2. Alimuuliza ajeacheze kwa karamu yake.
3. Hakukuja.
4. Aliamua kwamba Vashti hatakuwa mke wake tena. Atachagua malkia mpya kutoka kwa wanawake wa milki yake.
5. Mordekai ndiye alimlea binamuye yatima Esta.
6. Esta alikuwa mrembo. Mordekai alimpeleka kwa jumba la mfalme kama mfalme angweza kumchagua kama malkia mpya.
7. Mfalme Ahasuero alimchagua Esta kuwa malkia mpya.
8. Mordekai alisikia wanaume wawili wakipanga kumuua mfalme. Alipasha hiyo habari na wale wanaume wakauawa.
9. Jina la Mordekai liliandikwa kwa kitabu cha Mfalme cha kumbukumbu.
10. Mungu alipanga haya yote ili aokoe Wayahudi, watu wake.

## SHULE YA JUMAPILI YA CBM

**Awamu ya 1   Mwaka wa 3**



## 34 Esta anakuwa malkia

### Marejeo

Esta mlango wa 1: 1 – 3; 9 – 12 na 19 – 22. Esta mlango wa 2

### Kiini cha somo

Kuonyesha kwamba yatima Esta, aliyekuwa Myahudi anachaguliwa kama malkia wa Uajemi. Mungu alikuwa anapanga kuwaokoa Wayahudi, watu wake.

### Maneno maalum


- 34.1 Mfalme Ahasuero + karamu kubwa + itisha Vashti + karamu + hakuja
- 34.2 Mfalme anakasirika + Vashti + sio malkia + chagua malkia mpya + wajumbe +wanawake wazuri
- 34.3 Mordekai + Esta + mzuri + jumba la mfalme + Myahudi + Mfalme Ahasuero + Esta malkia mpya
- 34.4 Mordekai + watu wawili wanahila + Esta + ambia mfalme + watu waliuawa + kumbukumbu ya mfalme
- 34.5 Ilionekana kawaida + mpango wa Mungu + okoa watu wake + Wayahudi

**34.1** Mfalme Ahasuero alikuwa mfalme wa milki kubwa ya Uajemi. Siku moja alikuwa na karamu kubwa katika jumba la mfalme. Watu wa milki yake wa maana wote walialikwa. Kulikuwa na vyakula na vinywaji vingi vya kutosha kila mtu. Kila mtu alifurahi na kuburudika.

Mfalme Ahasuero alifikiri labda wageni wake watafurahi kumwona mkewe, Vashti akicheza. Kwa hivyo alituma mtumishi kumwita Vashti akujeacheze mbele ya wageni wake. Lakini Vashti alikuwa na karamu yake na marafiki wake akijiburudisha pia. Hakupenda aende mbele ya wageni wote wa mfalme naacheza. Kwa hivyo Vashti aliambia mtumishi kwamba hataenda.

**34.2** Mfalme alikasirika sana aliposikia hayo. Mbona Vashti akatae kucheza mbele yake! Ilimuharibia furaha ya karamu. Mfalme alikasirika sana na akasema hataki Vashti awe malkia tena. Atachagua malkia mwengine.

Wajumbe wa Mfalme walizunguka nchi nzima wakitafuta wanawake warembo ili wawalete kwa jumba la mfalme Shushani. Ililiwa Mfalme achague mmoja kama malkia mpya.



**34.3** Mordekai aliyejikuwa akifanya kazi kwa jumba la mfalme, alikuwa na binamuye msichana jina lake Esta. Wazazi wa Esta walikuwa wamekufa na Mordekai ndiye alimlea. Esta alikuwa mrembo sana. Mordekai alipeleka kwa jumba la mfalme ili awe mmoja wa wale mfalme anaweza kuchagua awe malkia mpya.


Mordekai alimwacha Esta kwa jumba la mfalme. Aliambia Esta kwamba asiambie mtu kwamba yeze ni Myahudi kwa sababu baadhi ya watu hawakupenda Wayahudi.

Esta aliishi kwa jumba la mfalme na wanawake warembo wenzake. Hawa wanawake walipewa nguo nzuri za kuva. Wangejichagulia kitu cho chote kizuri ili waonekane warembo mbele ya Mfalme.

Esta alipoenda kumwona Mfalme Ahasuero, alipendezwa sana na urembo wake mkuu. Tena alimpenda kwa sababu alikuwa mzuri na wa upendo. Mfalme alichagua Esta kama Malkia mpya.

**34.4** Mordekai alienda kila siku ili asikie habari ya Esta. Alikuwa na fahari kuu aliposikia kwamba Mfalme amemchagua Esta kama Malkia mpya. Lakini hakujitambua kwamba yeze ni binamu wa Esta.

Siku moja Mordekai alipokuwa akifanya kazi kwa Mfalme, alisikia watu wawili wakipanga kuua Mfalme Ahasuero. Pole pole Mordekai aliondoka. Alipelekea Esta huo ujumbe juu ya mpango wa wale watu. Kwa hivyo hiyo habari ilifikia Mfalme Ahasuero na wale watu wakauawa na Mfalme akapona. Mordekai alimwokoa Mfalme kwa kumwambia mpango wa wale watu. Jina la Mordekai liliandikwa katika vitabu vya Mfalme vya kumbukumbu.



**34.5** Mambo haya yote yalioneckana kama ya kawaida lakini yalikuwa yakipangwa na Mungu. Mungu alipanga haya yote na kuzudi lake – kuokoa Wayahudi, watu wake. Tutayaona kwa somolifwatalo.